

## **SALAAM ZA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA WANANCHI JUU YA UANZISHWAJI WA MFUKO WA FIDIA**

- Suala la Fidia ya ardhi ni miongoni mwa mambo muhimu kwenye utawala wa Ardhi. Usimamiaji sahihi wa masuala ya fidia huleta manufaa ya kiuchumi na kijamii na hivyo, kuiwezesha Serikali na wamiliki wa ardhi kunufaika na rasilimali muhimu ya ardhi. Kwa upande mwingine, utekelezaji wa Sera ya Taifa ya ardhi ya 1995 na Sheria ya Ardhi Na.4 ya 1999 unafanyika kwa hatua ili kukidhi matakwa yake chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, kuchelewa kutekelezwakwa Sera na Sheria imekuwa ni mojawapo ya changamoto zinazochangia uwepo wa migogoro inayohusiana na fidia nchini pamoja na kukwamisha utekelezaji wa majukumu mengi ya utawala na usimamizi wa ardhi.
- Kutokushughulikiwa kwa masuala ya fidia ipasavyo kumesababisha kutokuwepo kwa utawala bora katika sekta ya ardhi. Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 katika sehemu ya 4.2.19-20 inaainisha kuwa ardhi ina thamani, kipengele hiki kimeleta mwamko kwa wananchi kuitumia ardhi kama rasilimali na fursa ya kujiinua kiuchumi. Utwaaji wa ardhi na ulipaji wa fidia unapaswakuzingatia bei ya ardhi ya soko na viwango vya thamani katika ukokotoaji wa fidia. Pia uwazi, uadilifu na weledi wa wataalamu katika masuala ya fidia ni mambo ya muhimu sana.
- Kwa kutambua hili, Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 katika Fungu Na. 173 imeainisha uanzishwaji wa Mfuko wa Fidia unaosimamiwa na Bodi ya Wadhamini wa Mfuko w Fidia. Kimsingi sheria ilikusudia uwepo wa mfumo wa uwajibikaji kwa wahusika wote (Mtwaaaji ardhi na Mlipwa fidia) pamoja na uwazi katika utekelezaji wa masuala yote ya fidia. Ikumbukwe kwamba, malipo ya fidia yasiposimamiwa ipasavyo na kwa uwazi, huzungukwa na mianya ya rushwa kwa kuwanufaisha ama wataalam au wenye ardhi na Serikali ikiingia gharama zisizo za lazima kwa kutumia fedha za umma kwa hasara na pasipo tija. Kwa hiyo, ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeunda chombo cha kusimamia masuala yote ya ulipaji wa fidia nchini kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Mwongozo wa Kusimamia Mfuko wa Fidia ya Ardhi (*Operational Manual for Managing Land Compensation Fund*) nchini.

- Wadau wa Mfuko wa Fidia wako wengi kwa maana ya Taasisi/Mamlaka yoyote yenye nia ya kutwaa eneo kwa manufa ya umma ama matumizi mengine kwa kuzingatia sheria za nchi yetu. Hivyo ni rai yangu kwa wadau wote wa Mfuko kukitumia chombo hiki muhimu kwa manufaa ya wote kwa lengo la kuondoa kero na changamoto za ulipaji fidia.

## **SALAAM ZA MWENYEKITI WA BODI YA MFUKO WA FIDIA**

Bodi ya wadhamini ya kusimamia Mfuko wa Fidia ya Ardhi imeanzishwa kwa mujibu wa Kanuni za Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 (*The Land Management of the Land Compensation Fund Regulations, 2001*) ikiwa na Wajumbe 6.

Kazi za Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Fidia ardhi zimeanzishwa katika Kanuni ambazo zimetungwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, chini ya Vifungu Na. 173 na 179 vya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 82 la tarehe 4/3/2001. Kanuni hizo zinaitwa *The Land Management of the Land Compensation Fund Regulations, 2001*).

Kazi hizo ni:-

- (i) Kuwasilisha jedwali la Fidia na Madai mama litakvyowasilishwa na Kamishna wa Ardhi au Afisa Ardhi Mteule
- (ii) Kufanya Malipo ya Fidia kutoka kwenye Mfuko wa Fidia kwa kuzingatia taathmini halisi ya mali na ardhi kama itakavyothibitishwa na Mthamini mkuu wa Serikali.

Pamoja na majukumu hayo, majukumu mengine ni:-

- a) Kumshauri Waziri mwenye dhamana na Ardhi kuhusu vyanzo vipya vya Mfuko wa Fidia, marekebisho ya viwango vilivyopo vya fidia na kuhusu kanuni za ukusanyaji wa fedha za fidia;
- b) Kuhakikisha kunakuwepo na ukusanyaji, utunzaji na ulipaji wa fedha za fidia katika Akaunti ya Mfuko;
- c) Kutoa fedha kutoka kwenye Mfuko kulipa fidia kwa ajili ya utwaaji wa ardhi kwa Matumizi mbalimbali;
- d) Kufuatilia matumizi ya fedha za fidia zinazotolewa kwa ajili ya malipo ya fidia; na,
- e) Kutoa mapendekezo mengine yoyote kwa Waziri wa Ardhi yatakayoonekana ni muhimu ili kuiwezesha Bodi kutimiza majukumu yake.